


CHANJO HUOKOA MAISHA

Chanjo hutufanya tuwe na afya na kuokoa maisha.

Wakati mwingine huko Marekani, uthibitisho wa chanjo unaweza kuwa ni hitaji. Kwa mfano, unapopeleka watoto wako shuleni. Au kwa ajili ya kazi zingine na kutuma maombi ya uhamiaji.




Chanjo zimekuwepo kwa mamia ya miaka. Chanjo hutulinda dhidi ya magonjwa mengi hatari, kama vile surua, polio, mafua, COVID-19, na mengine.


Chanjo zimeokoa watu wengi zaidi kuliko uvumbuzi mwingine wowote wa matibabu.

Je, chanjo hufanya kazi kwa namna gani?


Chanjo ni salama na huzuia magonjwa. Huwa zinatayarisha mfumo wako wa kinga mwilini kugundua vijidudu kama bakteria au virusi.

Chanjo hufunza mwili jinsi ya kupambana na maambukizi yajayo kabla ya vijidudu kukufanya uwe mgonjwa. Kama vile mtoto anavyojifunza kusoma na kuandika, mfumo wa kinga mwilini husoma na kukumbuka maelezo kuhusu ugonjwa kutoka kwa kila chanjo.





Wakati, mara na dozi ya chanjo hutofautiana. Kwa mfano, chanjo zingine ni bora kuchukuliwa wakati mtu ni mchanga au mtoto. Zingine ukiwa mtu mzima, mzee au mjamzito.



Chanjo zingine unazihitaji mara moja tu. Zingine kila mwaka kama vile sindano ya mafua.

Kunaweza kuwa na chanjo za unaposafiri kwenda mahali fulani.

Je, una maswali kuhusu chanjo?

Zungumza na mtoa huduma wako wa afya. Wao wanaweza kukushauri vyema kuhusu chanjo ambazo wewe na familia yako mnahitaji.



Kumbuka: chanjo ni salama, zinafaa na zinaokoa maisha. Jamii nyingi huchukulia chanjo kama ishara za matumaini kwa maisha yajayo. Mojawapo wa njia bora zaidi tunaweza kujilinda sisi wenyewe na wapendwa wetu ni kwa kutumia chanjo. Zungumza na daktari wako leo!